

Kinda za battery

Mahali pa kutua

Mahali pa kutua ni muhimu kwa kuku kupumzikia ndani ya makaazi. Hutengenezwa kwa miti ya mviringo ya kimo wastani. Kila mti wa kupumzikia unaweza kutumika na kuku wazima watano.



Mahali pa kutua

Miti hii ni lazima itibiwe na mafuta taa ili kufukuza wadudu.

Usafi

Jenga vyumba ambavyo ni rahisi kusafisha ili kuzuia maradhi na wadudu.

Tumia majani au dawa ya kupe ili kuwauwa wadudu kutoka kwenye kuta na nyufa kila mara.

Kata nyasi na vijichaka vilivyo mita tatu pande zote za makaazi ili kuzuia nyoka na panya.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 5781 I, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Watayarishaji:

Wachira A.M. na Kithome J.N

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkuu wa Kituo,

KARI-Naivasha

S.L.P. 25, -20117, NAIVASHA

Simu: (050) 20165/6/7, 20748,20102

Nukulishi: (050) 20102

Baruapepe: karinaiv@kenyaweb.com

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 42 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Kuwajengea Kuku wa Kienyeji



Utangulizi

Kuku wa kienyeji hujengewa ili kuwapa makaazi kuku wenye kulalia mayai, kuku wenye kutaga mayai na vifaranga. Makaazi huwakinga ndege hawa dhidi ya adui zao na hali mbaya ya anga.

Mahali pa kujengea

Chagua sehemu iliyo na kivuli, mbinu za kuzuia upepo, jua kali na upepo mkali. Hakikisha pana usalama kutokana na adui wa kuku.

Nyumba zenye umbo la mstatili zinafaa kujengwa zikiangalia mashariki hadi magharibi ili kuepuka jua la alasiri.

Vifaa vya kujenga

Tumia vifaa vya kawaida kama miti, nyasi ya kuelekea nyumba, udongo au matofali.


- Bandua ngozi ya miti ambapo wadudu hupenda kujificha.
- Toa vifaa vyenye ncha kali kwenye nyumba.
- Madirisha ya kutosha ili kuingiza hewa.
- Tumia waya kwenye madirisha ili kuwakinga kutokana na adui.

Aina za makaazi

Aina ya makaazi ya kienyeji huwa ni;

Nyumba za kikapu

Hii ni nyumba ya kawaida inayojengwa kwa miti, waya au nyasi za mtoni. Inaweza kuchukua kuku 5 hadi 10 na inafaa kusongezwa kila siku.



Nyumba ya kikapu

Vikapu vya Vifaranga

Vikapu vya vifaranga huwakinga vifaranga dhidi ya ndege waliokomaa, maadui na hali mbaya ya anga. Kuku na vifaranga wanafaa kuishi na kula kwenye kikapu.

Makaazi ya sakafu ya mianya

Nyumba huinuliwa nusu mita kutoka kwenye ardhi ili kinyezi cha kuku kianguke chini. Sakafu hutengenezwa kwa kutumia miiti iliyoachana au waya ngumu. Weka kuku kumi kwa kila mita jumla.




Makaazi ya sakafu ya mianya

Makaazi ya Biwi (Deep litter)

Sakafu ya makazi haya hufunikwa na vifaa ambavyo vinalowa unyevu wa kinyezi cha kuku. Vifaa hivi ni kama vipande vya randa au nyasi. Weka kuku wanane kwa kila mita jumla.

Kiwanja cha kuku (Chicken Runs)

Hii ni sehemu wazi iliyojengwa ambapo kuku hutengwa dhidi ya adui. Jenga ukuta wa mita mbili wa udongo, miti au waya wa kuku. Kiwanja cha kuku hufaa sana wakati wa msimu wa kupanda, kwa kulisha, kuwapa maji na kutagia mayai.



Kiwanja cha kuku

Kinda au vitagio

Kinda hurahisisha uokotaji wa mayai safi. Hutengenezwa na vyungu vya udongo, vibuyu na vikapu vinavyoundwa na nyuzi, mbao na vijisanduku vya mbao.

Jenga kinda juu ya ardhi kwenye giza na utulivu. Kinda za battery huwa futi moja pande zote. Vifaa vya vitagio vinahitaji kubadilishwa mara moja kwa wiki.